**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** kila sifa njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma, kwa kutujaalia Uzima na Afya njema ambavyo vimetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili la Kumi kwa lengo la kuendelea kuwatumikia wananchi wetu. Vile vile, nachukuwa fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Barazakwa kuliongoza Baraza hili Tukufu kwa umahiri mkubwa na ninaamini kwamba mtaendelea kuliongoza Baraza hili kwa uadilifu wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, napenda kuchukuwa fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu, hali inayopelekea kupatikana kwa maendeleo pamoja na kuendelea kudumu kwa amani na utulivu katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inampongeza mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuteuliwa na mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais hatua ambayo inamfanya kuwa mmoja wa wasaidizi wakuu wa mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa shughuli za Serikali yetu.

**Mheshimiwa Spika,** pia, sina budi kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Saada Mkuya Salum kwa umahiri wake uliomfanya aweze kuteuliwa kushika nafasi hii katika Wizara hii mpya kimuundo pamoja na kuwapongeza watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu bila ya kuwasahau watendaji wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia makadirio ya Bajeti ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, nachukuwa fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisishia kazi yangu ya kuongoza kikao kuwa nyepesi zaidi, kwa hakika ni Wajumbe mahiri, wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha zinazoidhinishwa kwa Wizara hii zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima ya hali ya juu kabisa napenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |

| | | |
|---|---|---|
| *3.* | Mhe. Machano Othman Said | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *8.* | Ndg. Haji Jecha Salim | Katibu |
| *9.* | Ndg. Salma Muhsin Haji | Katibu |
| *10.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika kusimamia na kutekeleza Bajeti yake ina jumla ya Mafungu matatu *(3)* ambayo ni Fungu *B 01* – Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Fungu C O*4* – Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Usafirishaji wa Dawa za Kulevya na Fungu C O*5* – Tume ya Ukimwi.

## *FUNGU B 01:* OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha *2021/2022*, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Taasisi zake imelenga katika kukuza na kuwa sehemu ya ujenzi wa uchumi imara na salama, shirikishi, endelevu na himilivu kwa nia ya kupunguza umaskini, udhalilishaji, kasi ya maambukizi ya maradhi kwa mustakbali wa maendeleo ya taifa letu kiujumla.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya jitihada zinazofanywa na Idara ya Mazingira pamoja na Mamlaka ya Mazingira Zanzibar katika kuhakikisha uhifadhi na utunzaji wa

mazingira kuwa endelevu, Kamati imebaini kuna baadhi ya huduma za kijamii zinaondoa haiba ya muonekano wa mazingira na uoto wetu wa asili kama vile shughuli za uchimbaji holela wa mchanga, mawe, fusi hasa katika miradi mikubwa ya Serikali na kuacha mashimo makubwa bila ya kuyafukia pamoja na ujenzi holela katika sehemu hatarishi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inazishauri taasisi za Serikali zenye mnasaba na utunzaji wa mazingira zishirikiane katika kutunza uasili wa nchi yetu ili kizazi chetu na cha baadae kije kunufaika na mazingira mazuri.

**Mheshimiwa Spika,** pia, Kamati inashauri Serikali iipatie Mamlaka ya Mazingira Fungu *(Vote)* lake kama zilivyo mamlaka nyengine ili iweze kutekeleza vyema majukumu yake kwa wakati na ufanisi. Vile vile, Serikali inashauriwa kuchukuwa juhudi za kuijengea jengo la Ofisi Mamlaka ya Mazingira Zanzibar ili iendane na hadhi ya mamlaka za aina hii. Kamati pia, inaishauri Serikali kuharakisha kuifanyia marekebisho Sheria ya Mazingira ili iweze kwanda sambamba na mazingira yetu tuliyonayo.

**Mheshimiwa Spika,** usimamizi bora wa maendeleo unategemea pia suala la ujumuishwaji wa shughuli za watu wenye ulemavu katika mipango mbali mbali ya maendeleo ya nchi jambo ambalo Kamati yetu imeona utekelezaji wake kupitia Idara ya Watu Wenye Ulemavu. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya ukosefu wa taarifa sahihi, muhimu na zilizokamilika za watu wenye mahitaji maalum pamoja na shughuli wanazozifanya. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali katika sensa ya Taifa inayotarajiwa kufanyika mwaka wa fedha *2021/2022* kuwe na kipengele

maalum kwa ajili ya kukusanya taarifa hizo ili kurahisisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo na kuweza kuimarisha Mfumo wa Kielektroni wa watu wenye ulemavu uitwao *'Jumuishi Data Base'*.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, Kamati imebaini kuwa hakuna utaratibu maalum uliowekwa na Serikali wa kupata haki yao ya msingi ya elimu kutokana na kutokuwa na visaidizi vya kutosha vya watu wenye ulemavu. Hivyo, Kamati inashauri kulitafutia ufumbuzi sahihi suala hili kwani sote ni walemavu watarajiwa.

## ***FUNGU C 04:*** TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwepo kwa baadhi ya changamoto zinazoikabili Tume hii. Aidha, sote tunafahamu athari zinazotokana na uingizwaji, usambazwaji na utumiaji wa dawa za kulevya katika nchi yetu na duniani kwa ujumla. Kwa hakika nchi yetu inapoteza vijana wengi ambao ndiyo nguvu kazi ya taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuna changamoto kubwa ya kutopatikana kwa haki wakati wa kutoa hukumu za kesi za dawa za kulevya kwa kisingizio cha kupungua au kubadilika kwa vidhibiti *(ushahidi)*. Kamati inashauri kuwe na mashirikiano mazuri na yenye tija kati ya Tume pamoja na vyombo vya usimamizi na utoaji wa haki ikiwemo Polisi, Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahakama ili kutokomeza kabisa biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini mapungufu katika *Sheria ya Kudhibiti Usafirishaji wa Madawa ya Kulevya Nambari 9 ya Mwaka 2009* kwa Tume hii kutokuwa na nguvu katika utekelezaji wa majukumu yake. Hivyo, Kamati inashauri hii ifanyiwe marekebisho na kuwa Mamlaka ili kuipa uwezo na nguvu zaidi hasa wa kukamata watuhumiwa na kuwafikisha Mahakamani kwa lengo la kupambana kadhiya ya dawa za kulevya. Pia, Kamati inaishauri Tume hii iongeze wigo wa utoaji wa elimu kwa wanafunzi wa ngazi zote za kielimu ambapo idadi kubwa ya waathirika ni watoto na vijana ambao ndio ngao na nguvu ya maendeleo katikia taifa letu.

## ***FUNGU C 05:*** TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba matumizi ya dawa za kulevya na mapenzi ya jinsia moja *(Homosexual)* ni chachu ya ongezeko la maambukizi ya maradhi ya ukimwi kwa rika zote ambapo tafiti zinaonyesha asilimia Arobaini *(40)* ya waathirika ya *VVU* ni watumiaji wa dawa za kulevya. Hivyo, Kamati inaishauri Tume ya Ukimwi itoe elimu zaidi kwa jamii ili kuongeza kasi ya kupinga matumizi ya madawa za kulevya kwa nia ya kumaliza maambukizi ya Ukimwi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri *Sheria ya Adhabu, nambari 6 ya mwaka 2018* itumike katika vyombo vyetu vya kutoa haki ili kupunguza vitendo vya mapenzi ya jinsia moja na athari ya maambukizi ya virusi vya ukimwi.

## ***HITIMISHO***

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia hotuba yangu, nachukuwa fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati wote wa uwasilishaji wa maoni yetu. Aidha, Kamati inatoa shukrani zake za dhati kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndugu Raya Issa Msellem, Mratibu wa Kamati ndugu, Khamis Hamad Haji pamoja na watendaji wote kwa ujumla wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambao wamesaidia sana Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia Kamati imeona kwamba majukumu mengi ya taasisi za Serikali hayawezi kufanyika ipasavyo kutokana na kutoingiziwa fedha kwa wakati na kwa mujibu wa kilichopangwa katika bajeti zao. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati na kama zilivyopangwa ili ufanisi wa kiutendaji uweze kupatikana kwa maendeleo ya wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie Bajeti hii na hatimae waiidhinishe Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, makadirio ya fedha zilizopangwa kutumiwa kwa mwaka wa fedha *2021/2022*.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati yangu ***Naomba Kuunga Mkono Hoja.***

Ahsante,

**…………………………………**

**(Hassan Khamis Hafidh)**
Mwenyekiti,
Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar**